TANGAZO LA SERIKALI NA. 781 la tarehe 30/8/2024

SHERIA YA UHIFADHI WA WANYAMAPORI,
(SURA YA 283)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 121(a))*

## KANUNI ZA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA UVUVI KATIKA MAENEO YA HIFADHI ZA MWAKA 2024

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UTARATIBU WA MAOMBI YA KIBALI CHA KUFANYA SHUGHULI ZA UVUVI KATIKA MAENEO YA HIFADHI

3. Kibali cha shughuli za uvuvi.
4. Utaratibu wa maombi ya kibali.
5. Masharti ya kutoa kibali.
6. Muda wa kibali.
7. Ada ya kibali cha kuingia hifadhini.
8. Kibali cha chombo cha uvuvi.
9. Utaratibu wa maombi ya kibali cha chombo cha uvuvi.
10. Masharti ya kutoa kibali cha chombo cha uvuvi.
11. Ada ya chombo cha uvuvi.
12. Masharti ya chombo cha uvuvi.
13. Kutohamishika kwa kibali.

SEHEMU YA TATU
USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA UVUVI KATIKA MAENEO YA HIFADHI

14. Kuainisha maeneo ya shughuli za uvuvi.
15. Muda wa uvuvi.
16. Maegesho na matengenezo ya vyombo vya uvuvi.
17. Katazo la biashara ya mazao ya samaki.
18. Matumizi ya vyombo vya usafiri ndani ya maeneo ya hifadhi.
19. Masharti ya jumla.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI MENGINEYO

20. Kufutwa kwa kibali.
21. Rufaa.
22. Muda wa kufanya maombi ya kibali baada ya kufutwa.
23. Miongozo.
24. Adhabu ya Jumla.

MAJEDWALI

SHERIA YA UHIFADHI WA WANYAMAPORI,
(SURA YA 283)

KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 121)*

# KANUNI ZA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA UVUVI KATIKA MAENEO YA HIFADHI ZA MWAKA 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Usimamizi wa Shughuli za Uvuvi katika Maeneo ya Hifadhi za Mwaka 2024.

Tafsiri

2. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"eneo la uvuvi" maana yake ni eneo la maji katika maeneo ya hifadhi ambapo shughuli za uvuvi hufanyika;

"Kamishna wa Uhifadhi" itakuwa na maana sawa na iliyotafsiriwa chini ya Sheria;

"maeneo ya hifadhi" maana yake ni mapori ya akiba, mapori tengefu na maeneo mengine yanayosimamiwa na Mamlaka;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania;

"msimu wa uvuvi" maana yake ni muda wa kufanya shughuli za uvuvi uliopangwa na Mamlaka kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

Sura ya 283

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori;

"shughuli za uvuvi" zitajumuisha utafutaji, utegaji, uvuaji, ukamataji, ukusanyaji, uchakataji na usafirishaji wa samaki na mazao yake katika maeneo ya hifadhi; na

"Waziri" itakuwa na maana sawa na iliyotafsiriwa chini ya

Sheria.

Kibali cha shughuli za uvuvi

3.-(1) Mtu hataruhusiwa kufanya shughuli za uvuvi katika maeneo ya hifadhi bila kuwa na kibali cha kufanya shughuli za uvuvi kutoka kwa Kamishna wa Uhifadhi.

(2) Kibali cha kufanya shughuli za uvuvi kitakuwa kama kilivyoainishwa katika Fomu Na. 1 ya Jedwali la Kwanza.

(3) Mmiliki wa kibali, atatakiwa kuwa na kibali halisi au uthibitisho wa kibali muda wote akiwa ndani ya eneo lililohifadhiwa, na ataonesha kibali au uthibitisho wa kibali kwa afisa wa Mamlaka atakapotakiwa kufanya hivyo.

Utaratibu wa maombi ya kibali

4. Mtu anayekusudia kufanya shughuli za uvuvi katika maeneo ya hifadhi atatakiwa kuomba kibali kwa kujaza Fomu Na. 2 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Masharti ya kutoa kibali

5. Kamishna wa Uhifadhi anaweza kutoa kibali cha kufanya shughuli za uvuvi katika maeneo ya hifadhi endapo mwombaji-

(a) ni raia wa Tanzania;

Sura ya 279

(b) atawasilisha nakala halali ya leseni ya uvuvi iliyotolewa kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi;

(c) ametambuliwa na kuthibitishwa na uongozi wa Serikali ya Kijiji kilicho jirani na eneo la hifadhi ambapo shughuli za uvuvi zinafanyika; na

(d) amependekezwa na chama cha ushirika cha wavuvi katika eneo husika.

Muda wa kibali

6. Kibali cha kufanya shughuli za uvuvi katika maeneo ya hifadhi kitakuwa halali kwa muda wa msimu wa uvuvi.

Ada ya kibali cha kuingia hifadhini

7. Mmiliki wa kibali cha kufanya shughuli za uvuvi kilichotolewa chini ya Kanuni hizi atatakiwa kulipa ada ya kuingia kwenye hifadhi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Kibali cha chombo cha uvuvi

8.-(1) Mtu hataruhusiwa kutumia chombo cha uvuvi katika eneo la uvuvi bila kuwa na kibali cha chombo cha uvuvi kutoka kwa Kamishna wa Uhifadhi.

(2) Kibali cha chombo cha uvuvi kitakuwa kama kilivyoainishwa katika Fomu Na. 3 ya Jedwali la Kwanza.

(3) Mmiliki wa kibali cha chombo cha uvuvi atatakiwa kuwa na kibali halisi au uthibitisho wa kibali muda wote atakapokuwa akifanya shughuli za uvuvi katika maeneo ya hifadhi.

Utaratibu wa maombi ya kibali cha chombo cha uvuvi

9. Mtu anayetaka kutumia chombo cha uvuvi kwa ajili ya shughuli za uvuvi katika eneo la uvuvi ataomba kibali cha chombo cha uvuvi kwa Kamishna wa Uhifadhi kwa kujaza Fomu Na. 4 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Masharti ya kutoa kibali cha chombo cha uvuvi

10.-(1) Kamishna wa Uhifadhi anaweza kutoa kibali cha chombo cha uvuvi kitakachotumika katika eneo la uvuvi endapo-

(a) mwombaji ni raia wa Tanzania;
(b) chombo cha uvuvi kinamilikiwa na raia wa Tanzania;
(c) chombo cha uvuvi kimesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi; (Sura ya 279)
(d) chombo cha uvuvi kina urefu usiozidi mita 11; na
(e) chombo cha uvuvi kinatumia injini isiyozidi nguvu ya msukumo wa 40.

(2) Kibali cha chombo cha uvuvi kitatolewa kwa muda wa msimu wa uvuvi.

Ada ya chombo cha uvuvi

11. Mmiliki wa chombo cha uvuvi chenye kibali atatakiwa kulipa ada ya kutumia chombo cha uvuvi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Masharti ya kibali cha chombo cha uvuvi

12. Chombo cha uvuvi hakitaruhusiwa kuwa na wavuvi zaidi ya wanne wakati wa kufanya shughuli za uvuvi katika eneo la uvuvi.

Katazo la kuhamisha kibali

13.-(1) Kibali kilichotolewa chini ya Kanuni hizi hakiruhusiwi kuhamishwa kwa mtu mwingine.

(2) Mtu yeyote anayekiuka masharti ya kanuni hii anatenda kosa.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA UVUVI KATIKA MAENEO YA HIFADHI

Kuainisha maeneo ya shughuli za uvuvi

14. Kamishna wa Uhifadhi ataainisha maeneo kwa ajili ya shughuli za uvuvi katika maeneo ya hifadhi na kutoa taarifa kwa Halmashauri za Wilaya za maeneo husika.

Muda wa uvuvi

15.-(1) Uvuvi katika maeneo ya hifadhi utafanyika kuanzia mawio hadi machweo.

(2) Mtu atakayekiuka masharti ya kanuni hii anatenda kosa.

Maegesho na matengenezo ya vyombo vya uvuvi

16.-(1) Mamlaka inaweza kuainisha maeneo kwa ajili ya maegesho na matengenezo ya vyombo vya uvuvi.

(2) Mmiliki wa chombo cha uvuvi hataruhusiwa kufungua injini na kumwaga vilainishi vya vyombo vya uvuvi, aina yoyote ya mafuta, kutupa chupa, mifuko na vitu vingine vyovyote vinavyoharibu mazingira ndani ya eneo la hifadhi.

(3) Mtu yeyote anayekiuka masharti ya kanuni hii anatenda kosa.

Katazo la biashara ya mazao ya samaki

17. Mtu hataruhusiwa kuuza au kununua mazao ya samaki au kufanya biashara yoyote ndani ya eneo la hifadhi.

Matumizi ya vyombo vya usafiri ndani ya maeneo ya hifadhi

18.-(1) Matumizi ya vyombo vya usafiri ndani ya maeneo ya hifadhi kwa dhumuni la shughuli za uvuvi yataruhusiwa baada ya kulipa ada ya chombo cha usafiri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Vyombo vya usafiri vitakuwa-

(a) baiskeli; au

(b) gari.

(3) Gari lililoruhusiwa kuingia ndani ya eneo la hifadhi chini ya kanuni hii halitaruhusiwa kutembea kwa mwendokasi unaozidi kilomita 50 kwa saa.

Masharti ya jumla

19.-(1) Mtu anayefanya shughuli za uvuvi ndani ya eneo la hifadhi hataruhusiwa-

(a) kuingia au kutoka ndani ya eneo la hifadhi isipokuwa kwa kutumia njia zilizotengwa;
(b) kutoka nje ya eneo la umbali wa kilometa mbili kutoka kingo za mto, ziwa au bwawa la eneo alilopangiwa kufanya shughuli za uvuvi;
(c) kutumia vifaa vya uvuvi ambavyo havijaainishwa katika Kanuni hizi pamoja na leseni yake ya uvuvi;
(d) kuingiza spishi mpya ya viumbe maji ndani ya eneo la hifadhi;
(e) kuingiza wanyama wanaofugwa au ndege ndani ya eneo la hifadhi;
(f) kuingiza au kutumia aina yoyote ya milipuko, sumu au kemikali ndani ya eneo la hifadhi;
(g) kukata miti ndani ya eneo la hifadhi;
(h) kuingiza pikipiki ndani ya eneo la hifadhi;
(i) kutumia vibaya nyavu za uvuvi na kuzuia matumizi mengine ya maji katika eneo la hifadhi;
(j) kuvua spishi za samaki au viumbe maji vilivyokatazwa katika Sheria au Sheria ya Uvuvi; Sura ya 279
(k) kutumia kibali cha uvuvi kufanya shughuli za utalii;
(l) kufanya uharibifu wowote wa mazingira na uoto wa asili ndani ya eneo la hifadhi; na
(m) kuficha taarifa za uhalifu uliofanyika au unaopangwa kufanyika ndani ya eneo la hifadhi.

(2) Mtu yeyote atayekiuka masharti ya kanuni hii anatenda kosa.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI MENGINEYO

Kufutwa kwa kibali

20. Kamishna wa Uhifadhi anaweza kufuta kibali kilichotolewa chini ya Kanuni hizi endapo mmiliki wa kibali atakiuka masharti yoyote ya Kanuni hizi.

Rufaa

21.-(1) Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi uliotolewa na Kamishna wa Uhifadhi chini ya Kanuni hizi anaweza kukata rufaa kwa Waziri ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya uamuzi kwa kujaza Fomu Na. 5 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Waziri atatoa uamuzi wa rufaa iliyowasilishwa ndani ya siku ishirini na moja.

Muda wa kufanya maombi ya kibali baada ya kufutwa

22.-(1) Mtu aliyefutiwa kibali kilichotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi hataruhusiwa kufanya maombi ya kibali kingine kwa msimu unaofuata.

(2) Masharti ya kanuni ndogo ya (1) hayatatumika kwa mtu ambaye-

(a) atatiwa hatiani kwa makosa yaliyoainishwa katika Sheria;

(b) atatenda makosa yaliyoainishwa katika Kanuni hizi zaidi ya mara tatu ndani ya misimu miwili ya uvuvi.

Miongozo

23. Kamishna wa Uhifadhi anaweza kuandaa miongozo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa Kanuni hizi.

Adhabu ya jumla

24. Mtu atakayekiuka masharti ya Kanuni hizi anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua laki mbili na isiyozidi shilingi za kitanzania milioni moja au kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miezi sita au vyote.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 3(2), 4, 8(2), 9 na 21)*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

Picha

FOMU Na. 1

KIBALI CHA SHUGHULI ZA UVUVI KATIKA MAENEO YA HIFADHI

JINA LA ENEO LA HIFADHI: ...............................................................

Kibali hiki kimetolewa kwa ……………………………………….……………(Jina)
Namba ya simu……………………………………………………………………….
Anuani ya makazi Mkoa…… Wilaya……. Kata…... Kijiji…..Kitongoji………………
Kuanzia Tarehe ………/…………/……………. hadi ………/………/……………..
kufanya shughuli za uvuvi kwenye
bwawa/mto/ziwa…………………………….……………………………

Kiwango cha ada iliyolipwa…………………………………….
Namba ya Kumbukumbu ya malipo…………………………….
Namba ya risiti. …………….……….....  Tarehe ya malipo………………………....

…………………………….  …………………………
Saini ya mmiliki wa kibali  Saini ya Afisa aliyetoa kibali

Tarehe ……………………  Tarehe
………………..

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

Picha

FOMU Na. 2

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA UVUVI KATIKA MAENEO YA HIFADHI

JINA LA ENEO LA HIFADHI: ……………………………………………

SEHEMU A (Ijazwe na muombaji):

Jina: ………………………………..…………………
Namba ya simu: …………………..…………………
Anuani ya makazi (Mkoa, Wilaya, Kata, Kijiji, Kitongoji): ……………………………………................................
Namba ya Leseni ya Uvuvi: ………………………………
Mamlaka iliyotoa leseni: ………………………………..
Tarehe ya kutolewa kwa leseni ya uvuvi: …………………………………
Tarehe ya ukomo wa leseni ya uvuvi: ………………………………….

TAMKO LA MWOMBAJI
Ninatamka kwamba maelezo yaliyotolewa hapo juu ni ya kweli na ninaelewa masharti ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyampori na Sheria ndogo zilizotungwa chini ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori na ninatambua kwamba Mamlaka haitawajibika kwa madhara yoyote yatakayotokea kwangu nikiwa ndani ya eneo la hifadhi.

Saini: ………………………    Tarehe: ……………………………

SEHEMU B (Ijazwe na Chama cha Ushirika cha Mvuvi):
Jina la Chama…………………………………………………………
Anuani ya Chama: ……………………………………………………
Namba ya Usajili ya Chama: …………………………………………………
Jina la Mamlaka iliyosajili Chama ………………………………….

Maoni ya Chama (kama yapo) juu ya muombaji wa kibali
……………………………………………………………………………………....………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

Saini ya Katibu wa Chama ………………………. Tarehe …………………………..

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

FOMU Na. 3

KIBALI CHA CHOMBO CHA UVUVI KWENYE ENEO LA HIFADHI

JINA LA ENEO LA HIFADHI: …………………………………………..

Kibali hiki kimetolewa kwa …………………………………( Jina la Mmiliki wa chombo)
Namba ya simu: ………………….…………………
Anuani ya makazi (Mkoa, Wilaya, Kata, Kijiji, Kitongoji: …………………………………….
Jina la Chombo: ……………………….
Namba ya usajili: ……………………..
Namba ya leseni ya chombo cha uvuvi ………………………
Aina ya chombo: ………….……………………………
Kwa lengo la kufanya shughuli za uvuvi kwenye……………………………….…
Tarehe ya kutolewa kwa leseni ya chombo: …………………………………
Tarehe ya ukomo wa leseni ya chombo: ………………………………….

| | |
|---|---|
| ……………………………. | ………………………… |
| Saini ya Mmiliki wa chombo | Saini ya Afisa aliyetoa kibali |

Tarehe ……………………
Tarehe…………..

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

FOMU Na. 4

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA CHOMBO CHA UVUVI

JINA LA ENEO LA HIFADHI :………………………………………….

SEHEMU A (Ijazwe na muombaji):

Jina: ………………………………..…………………
Namba ya simu: …………………….…………………
Anuani ya makazi(Mkoa, Wilaya, Kata, Kijiji, Kitongoji): ………………………….
Namba ya leseni ya chombo cha uvuvi: ……………….........
Aina ya chombo: ………….……………………………
Mamlaka ya leseni: …………………………………..
Tarehe ya kutolewa kwa leseni ya uvuvi ………/……………/……………
Tarehe ya ukomo wa leseni ya uvuvi: ……/…………/………………….
Saini: ……………………… Tarehe: ……………………………

SEHEMU B (Ijazwe na Chama cha Ushirika cha Mvuvi):
Jina la Chama…………………………………………………………
Anuani ya Chama: ……………………………………………………
Namba ya Usajili ya Chama: …………………………………………………
Jina la Mamlaka iliyosajili Chama ………………………………….

Maoni ya Chama (kama yapo) juu ya muombaji wa kibali
………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

Saini ya Katibu wa Chama ………………………. Tarehe …………………………..

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

FOMU Na. 5

FOMU YA RUFAA

MAELEKEZO:

Itumwe kwa Mhe. Waziri wa Maliasili na Utalii ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya uamuzi.

1. TAARIFA ZA MRUFANI
   (i). Jina: ……………………………….…………………
   (ii). Namba ya simu: …………………….…………………
   (iii). Anuani ya makazi (Mkoa, Wilaya, Kata, Kijiji, Kitongoji): …………………….
   (iv). Aina ya maamuzi unayokatia rufaa: …………………………………………..
   (v). Sababu za rufaa:
   ……………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………
   (Unaweza kutumia karatasi ya ziada)

2. ORODHA YA VIAMBATISHO (Kama vipo)
   (i). …………….
   (ii). …………….
   (iii). ……………..

3. UTHIBITISHO
   Ninathibitisha kwamba maelezo yaliyotolewa hapo juu ni sahihi.

   Saini: ………………………   Tarehe: ……………………………

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7, 11 na 18(1))*

ADA

| N/A | Maelezo | | Kiwango cha Ada (kwa Shilingi za kitanzania) | |
|---|---|---|---|---|
| | | | PORI TENGEFU | PORI LA AKIBA |
| 1. | Ada ya maombi ya kufanya shughuli za uvuvi. | | 5,000/= | 5,000/= |
| 2. | Ada ya kibali cha kuingia hifadhini kwa ajili ya shughuli za uvuvi. | | 3,000/= kwa siku | 5,000/= kwa siku |
| 3. | Ada ya kibali cha kutumia chombo cha uvuvi kisichotumia injini hifadhini. | | 2,000/= kwa siku | 3,000/= kwa siku |
| 4. | Ada ya kuingiza baiskeli hifadhini kwa ajili ya shughuli za uvuvi. | | 1,000/= kwa siku | 2,000/=kwa siku |
| 5. | Ada ya kutumia chombo cha uvuvi kinachotumia injini. | 0 - 5 HP | 5,000/= kwa siku | 10,000/= kwa siku |
| | | 6 -15 HP | 10,000/= kwa siku | 20,000/= kwa siku |
| | | 16 - 25 HP | 20,000/= kwa siku | 30,000/= kwa siku |
| | | 26 - 40 HP | 30,000/= kwa siku | 50,000/=kwa siku |
| 6. | Ada ya gari kuingia hifadhini kwa shughuli za uvuvi. | Chini ya tani 2 | 5,000/= kwa safari moja kwa siku | 10,000/= kwa safari moja kwa siku |
| | | Tani 2 hadi tani 3 | 10,000/= kwa safari moja kwa siku | 20,000/= kwa safari moja kwa siku |
| | | Zaidi ya tani 3 hadi tani 7 | 20,000/ kwa safari moja kwa siku | 50,000/= kwa safari moja kwa siku |
| | | Zaidi ya tani 7 hadi tani 10 | 50,000/= kwa safari moja kwa siku | 100,000/= kwa safari moja kwa siku |

Dodoma,
13 Agosti, 2024

ANGELLAH J. KAIRUKI
*Waziri wa Maliasili na Utalii*